SCANNED

Hon. Chairs
For Tabling
2/4
06.05.21


| PAPERS LAID | |
|---|---|
| DATE | 11/05/2021 |
| TABLED BY | DSML. |
| COMMITTEE | — |
| CLERK AT THE TABLE | Daniel |

PARLIAMENT
OF KENYA
LIBRARY




# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA AKIHUTUBIA KIKAO CHA PAMOJA CHA BUNGE LA SENETI NA BUNGE LA TAIFA LA JAMHURI YA KENYA, NAIROBI, TAREHE 05 MEI, 2021

*Mheshimiwa Justin Muturi, Spika wa Bunge la Taifa;*

*Mheshimiwa Kenneth Lusaka, Spika wa Bunge la Seneti;*

*Waheshimiwa Wabunge la Taifa na Seneti;*

*Viongozi mbalimbali wa Serikali wa Tanzania na Kenya mliopo;*

*Wageni Waalikwa,*

*Mabibi na Mabwana.*

*Habari za mchana!*

## Shukrani kwa Bunge

**Waheshimiwa Maspika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia afya na

uhai na kutupa kibali kilichotuwezesha kukutana hapa siku ya leo.

Nina furaha kubwa leo hii kupata nafasi ya kuhutubia Kikao cha Pamoja cha Bunge la Taifa na Bunge la Seneti la Jamhuri ya Kenya. Kabla sijaendelea, niruhusu nitangulize shukrani zangu kwako Mheshimiwa Keneth Lusaka, Spika wa Bunge la Seneti na Mheshimiwa Justin Muturi, Spika wa Bunge la Taifa kwa kuitisha Kikao hiki cha Pamoja cha Bunge na kunialika mimi kukuhutubia. Kupitia kwenu niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Maseneta kwa kuridhia kwa kauli moja kufanyika kwa Kikao hiki. Asanteni sana.

Ninajiona mwenye bahati kubwa kupewa heshima hii adhimu na ya kipekee. Natambua fika kuwa huu si utaratibu wa kawaida wa Kenya. Si kila Rais anayefanya ziara rasmi hupewa heshima hii ya kuhutubia Bunge, tena Kikao cha Pamoja cha

Mabunge yenu mawili. Wenzetu mna Bunge lenye chemba mbili, sisi wenzenu, tuna moja tu. Kwangu itakuwa ndio mara ya kwanza kuhutubia Chemba mbili za Bunge kwa pamoja. Si jambo dogo. Mmenipa heshima kubwa sana. Nimefarijika kuwa nimepata nafasi hii mwanzoni mwa uongozi wangu. Niseme kuwa kumbukumbu hii daima haitofutika kwenye maisha yangu. Asanteni sana.

Uamuzi wenu wa kunipa fursa hii ni kielelezo cha thamani na uzito ambao mnaupa uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi zetu mbili. Niwahakikishieni kuwa nasi tumeguswa sana na heshima, upendo na ukarimu mkubwa ambao mmetuonyesha. Wema huacha deni, na deni la wema hulipwa kwa wema.

**Shukrani kwa Rais**

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Sitatenda haki nisipomshukuru kipekee Kaka yangu, ndugu yangu Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta. Rais Kenyatta ni miongoni mwa viongozi wa mwanzo kabisa aliyenipigia simu kunifariji mara tu baada ya kusikia taarifa ya kifo cha aliyekuwa Rais wetu Mpendwa, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kama haikutosha, hakusita kukatisha ratiba yake na kuweza kufika yeye binafsi kushiriki nasi katika msiba wa kitaifa kule Dodoma. Siku ile alitufariji sana kwa maneno yake na salamu zake za buriani kutoka kwa wananchi wa Kenya. Hatutasahau pia kwa kitendo chake cha kutukumbusha umuhimu wa kuheshimu dini na imani za wengine, pale alipositisha kuhutubia akiwa jukwaani ili kupisha adhana ya msikiti wa jirani iishe. Alituachia gumzo kubwa na funzo kubwa sana.

Alitumia jukwaa lile kunipongeza kwa kushika dhamana hii ya Rais wa Awamu ya Sita wa Tanzania na aliahidi kunialika

nchini Kenya mara baada ya kipindi cha maombolezo kumalizika. Rais Kenyatta ni mtu wa kutimiza ahadi. Mara tu baada ya kumaliza kipindi cha maombolezo, alinitumia Mjumbe Maalum kuniona, ambae mbali na mambo mengine, alileta mwaliko kwangu kufanya ziara rasmi nchini Kenya. Nami nimekuja Kenya kuitikia wito wake huo.

Mimi na ujumbe wangu tumepata mapokezi mazuri sana toka tumewasili jijini Nairobi. Tumejisikia tuko nyumbani haswa. Tumepokewa kwa ukarimu mkubwa, na hiyo ndio hulka, desturi na asili ya watu wa Kenya. Nimebaini kuwa, sehemu kubwa ya ujumbe niliombatana nao wanajua vichochoro vingi vya Nairobi, na msije kushangaa wengine wakatafuta sababu ya kubaki hapa.

Siku ya jana, nimefanya kikao na Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta na ujumbe wake wa viongozi wa Serikali. Tumekuwa na mazungumzo mazuri na yenye kuamsha matumaini makubwa

sana kwa mashirikiano kati ya nchi zetu kwa siku zijazo mbele yetu. Hapakuwa na ugumu wala ukakasi wowote katika kufikia muafaka wa mambo tuliyokuwa tukijadiliana. Tumezungumza kidugu sana.

Kilichojitokeza wazi katika mazungumzo yale, ni namna ambavyo nchi zetu mbili zinakubaliana katika mambo mengi kuliko yale machache sana tunayotofautiana. Hata hayo machache, tofauti zenyewe hazikuwa za msingi *(principles)* bali za mtazamo tu *(perceptions),* ambazo mara nyingi huchangiwa kutokana na kukatika kwa mawasiiliano baina ya pande zetu mbili. Ili kuondoa mitazamo hasi kati yetu, tumekubaliana kujenga na kuendeleza utamaduni wa kukutana mara kwa mara, katika ngazi mbalimbali. Ndugu na jirani wanaotembeleana hujenga ukaribu kuliko wale wasiotembeleana. ***Umbali hutengeneza mashaka. Ukaribu huyaondosha!***

## Madhumuni ya Ziara Rasmi Nchini Kenya

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Hii ni ziara yangu rasmi ya kwanza *(state visit)* tangu nilipoapishwa kushika nafasi ya Urais wa Tanzania tarehe 19 Machi, 2021. Ipendeze kusema kuwa, itaingia katika kumbukumbu za historia kuwa Kenya ndio nchi ya kwanza kwa Rais wa Awamu ya Sita wa Tanzania kufanya ziara rasmi. Kwa lugha nyingine, mguu wangu wa kwanza kutoka nje kwa ziara rasmi, umeanzia Kenya. Uamuzi wangu huu si wa bahati mbaya bali wa makusudi. Busara inaelekeza kuwa ukiwa 'mpangaji mpya' jitambulishe kwa majirani. Nilipata mialiko mingi, lakini nikasema nianzie hapa. Nimeanzia Kenya si kwa sababu ni karibu kijiografia, bali ni kwa sababu ya umuhimu na nafasi ya Kenya kwa Tanzania.

Uhusiano wa Tanzania na Kenya ni wa kipekee sana. Ni uhusiano uliofungwa katika mafundo matatu.

**Fundo** la kwanza ni udugu wa damu kati ya wananchi wetu wa pande mbili ambao hauwezi kutenganishwa na mipaka ya kuchora kwenye ramani. Makabila ya pande mbili za mpaka yanaingiliana na watu wake ni wale wale wamoja. Tanzania inapakana na nchi nane, lakini ni nchi ya Kenya pekee ndio ambayo tuna jamii nyingi zaidi zilizopo katika pande mbili za nchi zetu. Kwenye ukumbi huu kuna kina Otieno, Boke, Namelok kama ilivyo Tanzania. Kuna kina Kilonzo, Kioko kama ilivyo Tanzania. Kuna Mohammed Faki Mwinyihaji, Seneta wa Mombasa, lakini jina la Kizanzibari kabisa. Hii ni mifano michache sana.

**Fundo la pili** ni historia. Kabla hata ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1967, nchi zetu hizi

tayari zilishakuwa chini ya East Africa Common Services Organization (EACSO) zikiwa chini ya Utawala wa Kikoloni wa Waingereza. Huduma zetu muhimu, miundombinu yetu na chumi zetu zilishafumwa pamoja kabla hata nchi zetu hazijapata uhuru.

Na **fundo la tatu,** ni jiografia. Mwenyezi Mungu amejalia nchi zetu mbili hizi kuwa majirani. Tuna mipaka ya baharini na ardhini, na hata ikolojia yetu nayo ni moja. Ndio kusema kuwa, hata wanyamapori wetu ni ndugu na majirani, wakitoka Serengeti wanaingia Masai Mara. Siku hizi, hata Tausi wetu walioko Ikulu kule Tanzania, wana ndugu zao katika Ikulu ya hapa Kenya. *Kama Tausi wetu wana udugu, sembuse sisi watu wa Kenya na Tanzania?*

Kutokana na ukweli huu, ushirikiano wetu si wa hiyari bali ni wa lazima kutokana na kanuni ya uasili wa undugu ambao

M/Mungu ameuumba, ushirika na ujirani. Hili hatuna uwezo nalo wa kulibadilisha, tupendane ama tuchukiane, tuzungumze ama tununiane, hatuwezi kukwepana kutokana na mafundo haya matatu yaliyotuweka pamoja. Tunategemeana kwa kila hali - iwe kheri, iwe shari, iwe neema, iwe dhiki. Pakitokea ukame Tanzania, njaa inabisha hodi Kenya. Uzalishaji wa viwandani ukisimama Kenya, bidhaa zinakosekana Tanzania. Hivyo hapana budi ila tupatane na tuelewane ili tuishi pamoja kwa neema na furaha.

## Umuhimu wa Uhusiano wa Tanzania na Kenya

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Binafsi huwa nashangazwa sana na wale ambao wanadhani kuwa eti Kenya na Tanzania ni washindani, na hivyo uhusiano wetu unapaswa kuwa wa kuhasimiana na kukamiana.

Nawashangaa wanaodhani kuwa, Kenya peke yake, ama Tanzania peke yake, inaweza kuendelea bila mwenzake. Mbaya zaidi ni kule kuamini kwao kwamba, hilo linawezekana tu kwa mmoja wetu kumuangusha mwenzake. Hawa ni watu wenye mioyo ya choyo, maono mafupi na akili mbovu. Ni bahati mbaya kuwa watu hawa wapo katika pande zote mbili. Hutokea pia wachache wao wakawa ni Watumishi wa Serikali zetu na hata wanasiasa wa pande mbili za nchi yetu. Bahati nzuri tu ni kuwa si wengi na ndio maana uhusiano wa nchi zetu mbili umetimiza miaka 56.

Kwangu mimi, na katika Awamu yangu ya uongozi, nitahakikisha kuwa Kenya anabaki kuwa ndugu, jirani, mshirika wa mkakati na mbia. Kenya ni nchi ya **tano (5)** kwa nchi zinazoongoza kwa uwekezaji nchini Tanzania, nyuma ya Mataifa makubwa kama Uingereza, Marekani, China na India. Takwimu za Kituo chetu cha Uwekezaji (TIC) zinaonyesha kuwa, hadi

kufikia Machi 2021, kuna miradi ya uwekezaji 513 kutoka Kenya ambayo imetoa ajira 51,087 na kuchangia mapato ya kiasi cha **Dola za Kimarekani Bilioni 1.7 (USD milioni 1.713.56)** nchini Tanzania. Sekta zinazoongoza kwa uwekezaji kutoka Kenya ni uzalishaji viwandani, usafirishaji, kilimo, huduma, benki, ujenzi, rasilimali watu, madini, utalii na mali asili.

Kutokana na uhusiano wetu mzuri, kampuni za Tanzania zimewekeza nchini Kenya jumla ya miradi **thelathini (30)** iliyosajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji ya Kenya *(Kenya Investment Authority – KenInvest)*. Miradi hiyo ina thamani ya **Shilingi Bilioni 19.33 za Kenya** na kutoa ajira kwa raia wa Kenya 2,642. Si nyingi lakini si haba! Sekta inayoongoza kwa uwekezaji kutoka Tanzania ni sekta ya uzalishaji viwandani. Dhamira yangu ya kuja nchini Kenya, ni kuzungumza nanyi na kuona ni kwa namna gani Watanzania nao wataweza kufanya vizuri zaidi nchini Kenya.

Mbali na uwekezaji, ushirikiano wetu kwenye sekta ya biashara nao ni mkubwa na umeendelea kushamiri siku hadi siku. Usafirishaji wa bidhaa za Tanzania kwenda Kenya umeongezeka kutoka **shilingi za kitanzania Bilioni 390.6** mwaka 2017 hadi **shilingi za kitanzania Bilioni 526.3** mwaka 2020. Kwa upande wa Kenya, nayo iliongeza kiwango cha kuuza bidhaa zake nchini Tanzania, kutoka **shilingi za kitanzani Bilioni 420** mwaka 2017 hadi **shilingi za kitanzania Bilioni 571.1** mwaka 2020.

Takwimu hizi zinatusuta sisi viongozi na wanasiasa. Zinatuonyesha kuwa, wananchi wa nchi zetu mbili daima wako hatua mbele ya Serikali zetu. Wakati Serikali zetu zikisuasua, wananchi huendelea na biashara zao tena kwa ubunifu mkubwa kila mara. Ni wakati sasa wa sisi viongozi kubadilika. Tuwe daraja la kuwaunganisha watu wetu na sio tuwe kikwazo kwao.

Mimi na ndugu yangu Rais Kenyatta tumekubaliana tuweke utaratibu madhubuti wa kuzuia na kukabiliana na rabsha rabsha ambazo zimekuwa zinajitokeza hapa na pale na kuchafua hali ya hewa ya mahusiano ya kibiashara kati ya nchi zetu.

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Mashirikiano ya uwekezaji na biashara ni sehemu tu ya mashirikiano mazuri kati ya nchi zetu. Utalii ni eneo lingine ambalo tunapaswa kushirikiana sana. Kama nilivyogusia, ikolojia zetu zinaingiliana, vivyo hivyo ukaribu wa vivutio vyetu vya utalii. Tunayo nafasi ya kuneemeka pamoja ikiwa tutashirikiana katika sekta hii kuliko tukishindana. Badala ya kunyang'anyana idadi ya watalii, busara inatutaka tuelekeze nguvu zetu kuhamasisha mtalii aongeze idadi ya siku ambazo atazitumia nchini Kenya na Tanzania. Kwa kufanya hivyo tutapata sote.

Kama alivyowahi kusema hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, *"Tukipoteza muda mwingi kuwagawana kibaba, tutapoteza wasaa wa kuvuna pishi"*.

Mashirikiano yetu yanashamirishwa pia na jitihada kubwa tunazochukua katika vita dhidi ya uhalifu, ujangili, ugaidi, madawa ya kulevya na uharamia Bahari ya Hindi na katika Ziwa Victoria. Maadam wahalifu wa Kenya na Tanzania wana mashirikiano mazuri, basi hakuna budi vyombo vyetu vya ulinzi na usalama navyo viwe na mashirikiano mazuri zaidi kuwashinda wao. Mashirikiano haya mazuri baina ya vyombo vyetu, yamechangia sana kuwepo kwa utulivu na kutoa fursa kwa shughuli za biashara na uwekezaji kushamiri. Kenya ikiwa salama, nasi tunakuwa salama, hali kadhalika Tanzania ikiwa salama, Kenya mnakuwa salama.

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Ujenzi wa miundombinu ya pamoja ni sehemu ya jitihada zetu za kuimarisha mashirikiano yetu ya kiuchumi na kimkakati. Miradi hii inajumuisha kwa uchache:

i. Ujenzi wa barabara ya lami kutoka *Lamu – Mombasa – Tanga – Bagamoyo mpaka Dar es Salaam yenye urefu wa kilometa 454* chini ya Programu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kuendeleza Miundombinu ya Barabara kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East Africa Road Network Programme - EARNP)* katika Ushoroba wa Pwani *(Coastal Corridor)*. Kwa upande wetu tuko mbioni kukamilisha ujenzi wa kipande cha Pangani-Bagamoyo na barabara za lami zenye urefu wa **kilometa 124.5** na tayari tumekwishapata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

ii. **Barabara ya Arusha – Holili/Taveta - Voi yenye urefu wa kilometa 260.** Mradi huu ni sehemu ya mradi wa Maendeleo ya Barabara ya Arusha - Namanga – Athi River iliyofunguliwa rasmi mwaka 2012. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili na awamu ya kwanza imekamilika. Sasa tunajipanga kuendelea na awamu ya pili ya mradi huu.

iii. Tunavyo vituo vya Huduma za Pamoja Mpakani *(One Stop Border Post – OSBP)* vya Namanga - Namanga OSBP na Holili – Taveta OSBP. Vituo hivi vimerahisisha shughuli za biashara mipakani na uvukaji wa watu. Nafurahi kuona vituo hivi, vimekuwa chachu ya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mpaka wetu. Tunaendelea na mchakato wa kukamilisha mifumo ya vituo vya Horohoro –

Lungalunga OSBP na Sirari – Isebania OSBP ili navyo, viweze kutoa huduma kwa wepesi na ufanisi.

iv. Mradi wa kusafirishia umeme mkubwa wa **Kilovolti 400**. Kwa upande wa Tanzania mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka Singida hadi Namanga, ujenzi wa kituo kipya cha kupozea umeme mjini Arusha eneo la Lemugur na upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Singida. Kwa upande wa Kenya mradi unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa **Kilovolti 400** inajengwa kutoka kituo cha kupozea umeme cha Isinya hadi Namanga yenye urefu wa **Kilomita 96** itakayounganishwa na njia ya umeme inayojengwa upande wa Tanzania. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) pamoja na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) zimekubali kugharamia mradi huo.

v. Mwenyezi Mungu akijaalia, InshaAllah, Serikali zetu mbili zitaanza na kutekeleza mradi wa bomba la gesi kuitoa Dar es Salaam hadi Mombasa. Mazungumzo ya kutafuta fedha kwa ajili ya mradi huo yanaendelea na tunatarajia yatakamilika mapema iwezekanavyo.

Mtakubaliana nami kuwa, kwa ukubwa wa miradi hii, gharama zake na muundo wake unaolazimu nchi zetu mbili kushirikiana kuzijenga, ni ishara tosha kuwa uhusiano wetu si wa kuisha kesho, keshokutwa wala mtondogoo. Serikali zetu zinafanya uwekezaji huo kwa kuamini kuwa, uhusiano wetu upo vizuri na utaendelea kuwepo. Hivi ndivyo majirani na ndugu walioshibana wanavyoishi. Yeyote anayefikiria ama kudhamiria kuleta Uhasama baina yetu, Ujumbe kwao ni kuwa, Tanzania na Kenya tulikuwepo, tupo na tutaendelea kuwepo saana tu iwe masika, iwe kiangazi.

## Ushirikiano Kwenye Mapambano Dhidi ya COVID-19

*Waheshimiwa Spika, Waheshimiwa Maseneta na Wabunge*

Sote tunafahamu kwamba, Dunia inakabiliwa na janga kubwa la ugonjwa wa Korona, ambalo limeathiri kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zetu na limepelekea kwa sehemu kubwa kutulazimisha kubadili mfumo wetu wa maisha. Tunatambua kwamba kila nchi, ikiwemo Tanzania, imejiwekea utaratibu wa kupambana na janga hili kulingana na mazingira yake mahsusi na hali ya kusambaa kwa ugonjwa huo katika nchi hizo.

Niliwaeleza Watanzania katika hotuba yangu katika Bunge la nchi yetu, na napenda kurejea hapa, kwamba sisi Tanzania sio kisiwa, tunaishi kama sehemu ya familia ya jumuiya ya kimataifa. Kwa maana hiyo, kupitia Kamati ya Watalaam niliyoiunda, tumeanza mchakato wa kutafakari mbinu zaidi za kukabiliana na janga hili. Wakati tunaendelea kusubiri tumeendelea kuchukua

tahadhari zote ikiwemo kusitisha baadhi ya safari kwenye maeneo ya milipuko. Kwa vyovyote vile itakavyopendekezwa, jambo ambalo nina hakika nalo ni kwamba lazima tushirikiane na jirani zetu, ikiwemo Kenya, katika kukabiliana na janga hili. Mapambano dhidi ya janga hili yanapaswa kutuleta pamoja na sio kutufarakanisha. Ni imani yangu kwamba, tukiweka juhudi zetu na maarifa yetu pamoja, basi tutakabiliana na janga hili bila woga na tutashinda na maisha ya wananchi wetu yataendelea, huku tukichukua tahadhari.

**Uhusiano na Dhima ya Mabunge ya Tanzania na Kenya**

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Hatuwezi kuuelezea uhusiano wetu mzuri bila kutambua uhusiano wa Mabunge yetu ya nchi zetu mbili. Umekuwa ni uhusiano mzuri wa majira yote. Nitumie fursa hii kufikisha

kwenu shukrani za dhati za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa kuungana nasi na kutufariji katika kipindi kigumu cha msiba wa Hayati mpendwa wetu, Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mlitufuta machozi na mlitufariji sana. Tuliguswa sana na uamuzi wa Bunge la Seneti kupitia kikao chake cha tarehe 24 Machi 2021, kujadili na kusajili kwenye kumbukumbu za Bunge *(Hansard)* salamu maalum za rambirambi kufuatia kifo cha Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Nafahamu pia viongozi wa Mihimili Mitatu ya Serikali ya Kenya ukiwemo wewe Mheshimiwa Spika na Spika wa Bunge la Seneti, Mheshimiwa Keneth Lusaka mlitembelea makazi ya Balozi wetu kutoa salamu za pole. Sisi Watanzania tulifarijika sana kwa kuwa nasi wakati wa majonzi. Hatuna la kuwalipa ndugu zetu Wakenya zaidi ya kusema Mungu awabariki sana. Wakati wa msiba na dhiki ndio wakati mzuri wa kuwajua ndugu

zako wa majira yote. Mlitudhihirishia bila ya chembe ya shaka kuwa ninyi ni ndugu zetu wa shida na raha. Asanteni sana.

Sisi ni wafuatiliaji wakubwa wa mikutano ya Bunge la Kenya. Tunafanya hivyo kwa kuwa yanayojadiliwa humu, nasi yanatuhusu. Niseme tu kuwa Bunge la Seneti la Kenya na Bunge la Taifa la Kenya linatusisimua kwa mengi. Tunafurahia upana wa demokrasia yake, uzito wa mijadala yake, na hamasa ya Wabunge wake. Tulifurahishwa zaidi na uamuzi wenu wa kuanza kutumia Lugha ya Kiswahili. Halafu Kiswahili chenu pia kina vionjo vyake ambavyo peke yake ni burudani tosha! Tulifarijika sana kwa heshima kubwa mliyompa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai (Mb.) kuja nchini Kenya kuzindua Kanuni za Kudumu za Bunge la Kitaifa kwa ya lugha ya Kiswahili tarehe 31 Oktoba, 2019.

Rai yangu kwenu, ni kuwaomba mtusaidie kulea uhusiano wetu mzuri. Nasema hivyo nikitambua kuwa ninyi ndio wawakilishi wa wananchi na ndio sauti yao. Ninyi ndio wenye dhamana ya kutunga sheria, kushauri Serikali juu ya mwelekeo wa sera na kuwaongoza wananchi wenu waliowachagua. Dhima yenu katika kukuza ushirikiano baina ya nchi zetu ni kubwa sana. Mnao uwezo mkubwa wa kuamua kasi ya ushirikiano wetu iwe ya haraka ama ya kusuasua kwa aina ya sheria mtakazoamua kuzipitisha.

Dira na Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita ninayoiongoza ni ***"Kudumisha mazuri ya Awamu zilizopita, Kuyaendeleza mema yaliyopo na Kuleta mazuri mengine mapya" (stability, continuity and change).*** Hivyo, nimekuja kuwaahidi kuwa chini ya uongozi wangu, mimi na wenzangu tutafanya kila linalowezekana kuimarisha uhusiano kati ya nchi zetu mbili. Kama kuna palipolega katika uhusiano wetu, basi nimekuja hapa

Kenya ili kupakazia, na kule kulikokaza vizuri, nimekuja kupaimarisha.

## USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (EAC)

*Waheshimiwa Spika,*

*Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,*

Tanzania na Kenya ni wanachama waasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi zetu mbili ndizo zenye eneo kubwa kijiografia, idadi kubwa ya watu na milango pekee ya bahari kwa nchi zingine za Afrika Mashariki.

Ukweli huu unakuja na wajibu na dhima kubwa kwa nchi zetu mbili. Uhusiano wa nchi zetu mbili ukishamiri, Afrika Mashariki nzima inashamiri. Biashara kati yetu ikistawi, Afrika Mashariki nzima inastawi. Hivyo basi, hatuna budi nchi zetu mbili kutambua wajibu wetu na dhima yetu hiyo kwa Afrika

Mashariki. Tunapaswa tutambue kuwa kila mara panapotokea kutoelewana kati yetu, tunadhoofisha Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Bila kukusudia, tunajikuta pia tunaathiri kasi ya utangamano wa Afrika Mashariki.

Nikiri kwamba, kuna nyakati ambapo ushirikiano wa Afrika Mashariki ulijaribiwa, ambapo baadhi ya matukio, kauli na vitendo vyetu viliyaweka majaribuni mahusiano yetu na kuupima uimara wa dhamira yetu ya kuendelea na safari yetu ya utangamano. Ninachofarijika ni kwamba katika nyakati zote hizi, kwa busara za viongozi waliotutangulia na kwa uimara ya mafundo ya uhusiano wetu, tulishinda na dhamira yetu iliimarika zaidi. Uchungu wowote uliojitokeza pale tulipojaribiwa ulikuwa uchungu wa uzazi, sio uchungu wa maradhi. Uchungu wa uzazi huishia kwenye furaha.

Niwahakikishie kuwa, mimi na wenzangu nchini Tanzania, tutafanya kila linalowezekana ili uhusiano wetu uzidi kung'ara, na kwa kufanya hivyo, tung'arishe ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tanzania itaendelea kuwa jirani, mbia na rafiki mwaminifu wa Kenya na mwanachama mwadilifu na wa kutumainiwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jitihada zangu na wenzangu katika Serikali ninayoiongoza zitaelekezwa katika kuimarisha ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tutaelekeza jitihada zetu katika kutafuta majawabu palipo na changamoto, kufufua fursa palipo na vikwazo na kuleta matumaini palipo na mashaka. Tutafanya hivyo kwa kuamini kwa dhati kabisa kuwa, sisi Wana Afrika Mashariki, ***Hatma yetu imefungamana. Nasi hatuna budi tutangamane.***

Ombi langu kwenu Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie kutuhimiza sisi tulioko Serikalini tutekeleze wajibu wetu huu

adhimu. Pale tunapolega, msisite kutukosoa. Nanyi pia tunawaomba mtimize wajibu wenu. Mtusaidie kutunga sheria na kushawishi Serikali zenu kuhusu sera zinazochochea na kuwezesha utangamano. Tusiruhusu na tukemee misimamo, mitazamo na kauli za baadhi ya wanasiasa ndani na nje ya Bunge ya kuleta mgawanyiko na kudhoofisha Jumuiya yetu. Daima, tuwatangulie wafanyabiashara na wananchi wetu katika utangamano na kuwaongoza, badala ya ninyi Waheshimiwa Wabunge kuwavuta nyuma na kuwakwamisha. Kwani falsasa zinasema, ***kuongoza ni kuonyesha njia! Na sio kufunga njia"***

**Hitimisho**

***Waheshimiwa Spika,***

***Waheshimiwa Maseneta na Wabunge,***

Kama mjuavyo, ***"moyo ukielemewa na furaha, hucheulia mdomoni"***. Ningetamani kuendelea kuzungumza kwa kirefu

sana kuelezea furaha yangu kwa upendo mkubwa mlionionyesha, ukarimu mkubwa mlionifanyia na heshima kubwa mliyonipa. Isitoshe, maneno ya kuzungumza nayo pia ni mengi ikizingatiwa upana, ukubwa na uzito wa uhuasiano wa nchi zetu mbili. Jambo zuri ni kwamba Watanzania na Wakenya wakikutana hawamalizi maongezi, huwa tunaahirisha tu maongezi na kuyaendeleza tunapokutana tena. Utani humo humo. Vijembe humo humo. Ndio mambo yanayochangamsha uhusiano wetu. Sina shaka kuwa tutapata fursa ya kuyazungumza mengi kwa kina katika majukwaa mengine tutakayokutana.

Nitumie fursa hii kumshukuru kwa mara nyingine tena, Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta kwa mwaliko wa kufanya ziara ya Kiserikali nchini Kenya. Nami nimemualika aje kututembelea na kupata fursa ya kula makande ya Tanzania nyie

mnaita githeri. Nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge la Seneti Mheshimiwa Kenneth Lusaka na Spika wa Bunge la Taifa Mheshimiwa Justin Muturi. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Maseneta kwa kutenga muda wenu adhimu kunikaribisha kuzungumza nanyi. Kupitia kwenu, niwashukuru ndugu zetu wananchi wa Kenya kwa mapokezi mazuri mliyotupatia. Tunaondoka Kenya na kumbukumbu nzuri za ziara hii na shauku kubwa ya kurudi tena siku zijazo.

Hii ni ziara yangu ya kwanza nchini Kenya. Nawaahidi kuwa haitakuwa ya mwisho.

*Udumu undugu wa Wakenya na Watanzania.*

*Wadumu viongozi wetu.*

*Mungu Ibariki Jamhuri ya Kenya.*

*Mungu Ibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Asanteni sana kwa kunisikiliza!